**4.4. MATAKWA YA KISHERIA BAADA YA USAJILI**

1. Kulipa ada ya mwaka Shs 100,000/=;
2. Kuwasilisha taarifa ya hesabu za fedha iliyokaguliwa kwa Mkurugenzi Mkuu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kila mwaka;
3. Kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya chama kwa kila mwaka;
4. Kuwasilisha taarifa ya mihutasari ya mkutano mkuu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kila mwaka.

**5.0. UONGOZI WA VYAMA**

Uongozi wa vyama vya wakulima wamwagiliaji utajumuisha kamati ya usimamizi na ka-
mati nyingine ndogo.

**5.1 Kamati ya usimamizi:** Uongozi wa juu wa chama ni Kamati ya usimamizi yenye wajumbe wasiopungua 5 na wasiozidi 9 waliochaguliwa miongoni mwa wanachama.

**5.2 Kamati ndogo muhimu**; katika vyama vya wakulima wamwagiliaji:
Chama cha wakulima wamwagiliaji kinaweza kuwa na kamati nyingi kulingana na mahitaji yao. Kamati ndogo za msingi ambazo ni lazima ziwepo katika muundo wa uongozi wa vyama vya wakulima wamwagiliaji ni:-

- Kamati ndogo ya Utawala, Mipango na Fedha;
- Kamati ndogo ya Kilimo na Mazingira;
- Kamati ndogo ya Maji, Uendeshaji na Matunzo.
- Kamati ya usuluhishi wa migogoro

Kanuni ya 97 ya sheria ya umwagiliaji inaelekeza uundaji wa kamati ya usuluhishi wa migogoro yenye wajumbe wasiopungua 3 na wasiozidi 5 waliochaguliwa miongoni mwa wanachama. Wajumbe wa kamati ya usuluhishi wa migogoro watachaguliwa katika mkutano mkuu ambao hawatatokana na wajumbe wa kamati kuu ya Usimamizi.

**5.3. Katazo la Uongozi:** Kwa mujibu wa kanuni ya sheria (2015) ya 18 (1) inakataza viongozi wa kisiasa na kidini kuwa miongoni mwa viongozi katika vyama vya wakulima wamwagiliaji.



**5.3. VIINGILIO NA MICHANGO YA LAZIMA KWA WANACHAMA**

- Viingilio wakati wa kujiunga na chama;
- Ada ya mwaka kwa mwanachama
- Ada ya Huduma za Umwagiliaji ambayo ni asilimia tano (5%) ya wastani wa mavuno kwa ekari katika skimu husika.

**Ada hii ni kwaajili ya ;-**

- Kusaidia vyama vya wakulima wamwagiliaji kuweza kumudu gharama za uendeshaji na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji, ikiwa ni kufanya shughuli za ukarabati mdogo kama vile; kupaka vilainishi kwenye mageti ya banio, kupaka rangi kwenye mageti na kuziba nyufa kwenye mifereji kwa wakati pale tatizo linapojitokeza;
- Uendeshaji wa ofisi za vyama vya wakulima wamwagiliaji;
- Kulipa watendaji wa ofisi za vyama vya wakulima wamwagiliaji; na
- Kugharamia shughuli zozote zitazojitokeza.

**6.0. UKAGUZI WA HESABU ZA FEDHA**

Kanuni za Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji za mwaka 2015 zimeweka sharti kwa vyama vyote vya wakulima wamwagiliaji kuwasilisha taarifa za hesabu za fedha zilizokaguliwa kwa Mkurugenzi Mkuu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji.

**6.1. Ukaguzi wa ndani:**
Ukaguzi huu unaweza kufanywa na kamati ndogo ya mipango na fedha au chama cha wakulima wamwagiliaji kinaweza kumteua mwanachama au mtu yeyote mwenye uwezo wa kufanya kazi hiyo.

**6.2. Ukaguzi wa nje:**
Ukaguzi wa nje utafanywa na wakaguzi waliosajiliwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA).


**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**

**S.L.P. 146, Njedengwa Dodoma**

**Simu:** +255 26 296 2073

**Barua Pepe:** info@nirc.go.tz

**Facebook/Instagram/Twitter:** Nirc_tz

**Youtube:** Tume ya Taifa ya Umwagliaji

**Tovuti:** www.nirc.go.tz


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI**

# USAJILI WA VYAMA VYA WAKULIMA WAMWAGILIAJI

## 1.0 UTANGULIZI

Vyama vya wakulima wamwagiliaji ni muungano wa wakulima wenye nia moja ya kuendeleza Kilimo cha Umwagiliaji katika skimu kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao kwa kuzingatia usimamizi wa matumizi ya maji, kusimamia shughuli za uendeshaji na matunzo katika skimu za wakulima wamwagiliaji.
Vyama vya wakulima wamwagiliaji ni muhimu kwa kuwa ndio chombo kinacho simamia shughuli za Uendeshaji na Matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji ili skimu za umwagiliaji ziweze kuwa endelevu. Ujenzi wa miundombinu ya skimu za umwagiliaji hugharimu fedha nyingi za serikali hivyo bila kuwa na chombo maalum kwaajili ya kusimamia Uendeshaji na Matunzo ya skimu muda wa uhai wa skimu huwa mfupi kuliko ilivyotegemewa.

## 2.0. MADHUMUNI YA UANZISHWAJI WA VYAMA VYA WAKULIMA WAMWAGILIAJI

Madhumuni ya vyama vya wakulima wamwagiliaji yamebainishwa wazi katika sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2013 kifungu cha 30; sheria hii imeonyesha kwamba madhumuni ya vyama vya wakulima wamwagiliaji yatajumuisha:-

- Kuhamasisha na kuhakikisha usawa kwa wamwagiliaji,
- Kuelimisha juu ya uhifadhi wa maji, utunzaji bora wa mifumo ya umwagiliaji, ufanisi na matumizi bora ya maji kwa ajili ya uzalishaji wa mazao; na
- Kutunza mazingira na kuhakikisha uwiano wa kimazingira kwa kushirikisha wakulima

## 3.0. MAJUKUMU YA VYAMA VYA WAKULIMA WAMWAGILIAJI

Kifungu cha 31 cha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2015 kinaelekeza kwamba vyama vya wakulima wamwagiliaji vitatekeleza majukumu yafuatayo: -

- Kuandaa na kutekeleza ratiba ya umwagiliaji kwa kila msimu wa umwagiliaji; inayoendana na mpango wa uendeshaji kwa kuzingatia kibali cha matumizi ya maji;
- Kuandaa mpango kwa ajili ya uendeshaji na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji kila mwisho wa msimu;
- Kusimamia matumizi ya maji na ardhi katika mfumo wa umwagiliaji;
- Kuhamasisha matumizi ya maji kwa ufanisi na ugawaji maji;
- Kukusanya Ada ya Huduma za Umwagiliaji;
- Kutunza daftari la orodha ya wanachama wa chama cha wakulima wamwagiliaji;
- Kuandaa na kutunza taarifa za mifumo ya umwagiliaji ikijumuisha mali na madeni katika skimu za umwagiliaji;
- Kutatua migogoro baina ya wanachama katika skimu za umwagiliaji;
- Kusababisha na kutunza vitabu vya hesabu zilizokaguliwa kwa kila mwaka;
- Kufanya mapitio, ufuatiliaji na tathmini ya utekezaji wa mara kwa mara na ugawaji wa maji;na
- Kutekeleza majukumu yoyote mengine kama yatakavyoainishwa na katika katiba

## 4.0. UANZISHAJI WA VYAMA

Mchakato wa uanzishwaji wa vyama vya wakulima wamwagiliaji huwezeshwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kama inavyobainishwa katika kifungu cha 29 (1) cha sheria ya umwagiliaji)
Chama cha wakulima wamwagiliaji huanzishwa na wakulima kuanzia kumi na kuendelea wanaojihusisha na kilimo cha umwagiliaji katika eneo husika.
Kwa mujibu wa sheria ya Taifa ya Umwagiliaji namba 4 2013, wakulima wote wenye mashamba katika eneo la umwagiliaji wanatakiwa kuwa wanachama wa chama cha wakulima wamwagiliaji.

## 4.1. USAJILI WA VYAMA VYA WAKULIMA WAMWAGILIAJI

Vyama vya wakulima wamwagiliaji huasajiliwa kwa mujibu wa sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4 2013 na kanuni zake za 2015. Vyama vyote vya wakulima wamwagiliaji vinatakiwa kusajiliwa na kutambulika kisheria.

## 4.2. MATAKWA YA USAJILI

1. Nakala nne (4) za fomu ya maombi iliyojazwa (NIA)
2. Nakala nne (4) za katiba;
3. Nakala nne (4) za picha kwa saizi ya pasipoti kwa wajumbe wa kamati ya uanzilishi na maelezo yao;
4. Nakala nne (4) za muhtasari uliopitisha katiba ukiwa unaonyesha majina kamili na saini za wajumbe waliohudhuria kwa wino mbichi;
5. Nakala nne (4) za barua ya kuungwa mkono kutoka Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
6. Nakala nne (4) za barua ya maombi ya usajili ikiwa imepigwa muhuri na kusainiwa na Mwenyekiti na Katibu wa chama cha wakulima wamwagiliaji;
7. Nakala nne (4) za orodha ya wanachama waanzilishi na saini zao kwa wino mbichi;na
8. Ada ya Usajili shilingi 175,000/=

## 4.3. ADA ZA USAJILI WA CHAMA CHA WAKULIMA WAMWAGILIAJI

**Kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na 4 ya mwaka 2013 kifungu cha 39, aya ya 9 ya kanuni za umwagiliaji za mwaka 2015 zinaipa mamlaka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kukusanya Ada mbalimbali zilizoainishwa katika Jedwali la pili la kanuni za Sheria ya Umwagiliaji.**

| NA | AINA YA ADA | KIASI | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya maombi ya usajili (Application fee) | 15,000 | Ada hii ya maombi ya usajili wa chama hulipwa pale chama kinapotuma maombi ya Usajili Tume ya Taifa ya Umwagiliaji |
| 2 | Ada ya usajili (Registration fee) | 60,000 | Ada hii ni kwaajili ya kugharamia mchakato mzima wa usajili wa chama ndani ya Tume |
| 3 | Ada ya mwaka (Annual fee) | 100,00 0 | Ada hii hulipwa kila mwaka kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kuhuisha uhai wa chama |
| 4 | Ada ya mabadiliko ya katiba/sheria ndogo za vyama vya wa wakulima wamwagiliaji. | 25,000 | Kabla ya kufanya mabadiliko yeyote ya neno/ kifungu/ sentensi katika katiba na sheria ndogo za vyama vya wakulima wamwagiliaji, vyama vya wakulima vitawajibika kutoa taarifa kwa Mkurugenzi mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. |
| 5 | Ada ya mabadiliko ya jina la chama | 25,000 | Mabadiliko yeyote ya jina la chama katika katiba za vyama vya wakulima wamwagiliaji, vinatakiwa kutoa taarifa kwa Mkurugenzi mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. |
| 6 | Faini ya ucheleweshaji wa taarifa za mwaka za ukaguzi wa hesabu za fedha, taarifa ya maendeleo ya chama na muhtasari wa mkutano mkuu wa mwaka | 100,00 0 | Kushindwa kuwasilisha taarifa hizo kwa wakati kunapelekea kutozwa faini ya ucheleweshaji. |
| 7 | Adhabu ya uchelewashaji wa ada ya mwaka | 40,000 | Kushindwa kulipa ada ya mwaka kwa wakati. |